

**SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WAFANYAKAZI TANZANIA
(TUCTA)**

**SALAMU ZA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WAFANYAKAZI
TANZANIA (TUCTA) ZILIZOTOLEWA NA NDUGU TUMAINI
NYAMHOKYA MKUNDA, RAIS MKUU WA TUCTA KWENYE KILELE
CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA DUNIANI, 28
APRILI, 2022 DODOMA.**

**Mh. Prof Joyce Ndalichako, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira
na Vijana,**

**Mh. Patrobas Katambi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira
na Vijana,**

Mh. John Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma

**Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Kanda ya Afrika
Mashariki.**

**Ndugu Suzan Ndomba, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri
Tanzania (ATE).**

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi,

Ndugu Wafanyakazi,

Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mgeni Rasmi.

Leo ni siku ya kuwakumbuka wafanyakazi wenzetu walioumia, kupata ulemavu na wengine kufariki kutokana na ajali au magonjwa wakati wakiwa kazini. Siku hii hutupatia fursa ya kutafakari hali madhara yanayotusibu sehemu zetu za kazi na namna ya kujikinga dhidi ya madhara hayo.

Kwa jumla sehemu za kazi zina vihatarish vingi na haziko salama kwa kiwango kinachotakiwa. Ukweli huu unadhihirishwa na takwimu mbali mbali pamoja na matukio ya ajali na maafa yanayotokea katika machimbo, viwandani na mashambani ambapo wafanyakazi wanaumia na wengine wanapoteza maisha kwa sababu ya vihatarishi vinayotokana na kazi zisizo salama au mazingira yasiyo salama.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kwa kuzingatia Kauli mbiu ya maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya mwaka huu ambayo ni; **KWA PAMOJA TUSHIRIKIANE KUJENGA PA KAZI.** Ni dhahiri kuwa sote tunapaswa kushirikiana kikamilifu katika kujenga na kuimarisha Mifumo ya Usalama na Afya mahali pa kazi ili kujikinga na kuzuia athari mbalimbali zinazojitokeza. Aidha kuitumia Mifumo hiyo ya Usalama na Afya kutujengea tabia na mienendo yetu kazini ndiyo kuwa utamaduni wetu shughuli zetu mahali pa kazi.

Sera ya Taifa ya Uchumi wa Viwanda na Uwekezaji ni moja ya jitihada za Serikali ambazo zitatunufaisha kiuchumi kwa upande mmoja lakini pia kuna vihatarishi vya kila aina vitokanavyo na viwanda kwa upande mwingine. Vihatarishi vitokanavyo na uzalishaji katika viwanda husababisha changamoto nyingi za kiusalama na magonjwa.

Hivyo ni vizuri kujizatiti zaidi katika kuimarisha Mifumo madhubuti ya Usalama na Afya mahali pa kazi ili kuepusha athari kwa wafanyakazi na waajiri wao.

Serikali, Waajiri na Wafanyakazi wote tunao wajibu wa kuhakikisha kuwa sehemu zetu za kazi ni salama. Hivyo, **ninapenda kutoa wito, kuwa wote tushirikiane kuhakikisha kuwa tunatimiza** wajibu wetu kwa kila mdau kuhakikisha kuwa mahali pa kazi pako salama.

Kwa upande wa Serikali ni wajibu wake na tunakumbusha kutekeleza mambo yafuatayo:

- i. Kuelekea uchumi wa Viwanda Serikali ihakikishe kwamba wawekezaji wote wanaokuja hapa nchini wanatimiza masharti ya Usalama na Afya kazini sambamba na shughuli wazifanyazo.
- ii. Serikali ipanue wigo wa elimu ya ufundi (Polytechnic Colleges) inayoshabihiana na uchumi wa Viwanda na kuweka Mitaala ya elimu ya Usalama na Afya katika mafunzo hayo pamoja na Shule za Sekondari.
- iii. Serikali iweke na kusimamia utaratibu ulio salama katika kuondoa (disposal) kemikali zenye sumu pamoja na kuhifadhi mazingira salama, ili kuzuia ongezeko la athari zitokanazo na uzalishaji Viwandani.

Kwa upande wa Waajiri, tunahimiza watekeleze yafuatayo:-

- i. Waanzishe na kuimarisha mipango ya mafunzo juu ya Afya na Usalama kwa wafanyakazi wao.
- ii. Waweke utaratibu wa ukaguzi wa afya wa mara kwa mara (periodic medical examination) kwa wafanyakazi wao.

- iii. Vilevile waunde Kamati za Afya na Usalama katika sehemu zote za kazi hapa nchini na kuhakikisha kwamba zinafanyakazi ya kuboresha Usalama na Afya wa Wafanyakazi.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Katika miaka kadhaa ya uhai wa Mamlaka ya Wakala wa Afya na Usalama (OSHA) tumeshuhudia maboresho na kuimarika kwa Mifumo ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Ukaguzi unaofanywa na OSHA kuchunguza Mifumo, Mitambo, kupima wafanyakazi mara kwa mara pamoja na kutoa Elimu na Ushauri kumesaidia kwa kiasi kikubwa sana katika kuimarisha usalama na Afya kwa wafanyakazi na waajiri mahali pa kazi.

Napenda nitumie nafasi hii kupongeza viongozi na wafanyakazi wa Mamlaka ya Wakala wa Usalama na Afya (OSHA) kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kuchangia kuboresha hali ya usalama mahali pa kazi.

Mwisho ninamalizia kwa kusema kuwa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) kwa kushirikiana na wafanyakazi wote nchini linaahidi kuwa litashirikiana kikamilifu wakati wote katika jitihada zote za Serikali na Mamlaka ya OSHA kuhakikisha kuwa tunajenga Utamaduni wa Usalama na Afya mahali pa kazi ili kulinda nguvu kazi kwa maendeleo ya taifa letu.

NAWASHUKURU KWA KUNISIKILIZA.

RAIS - TUCTA